



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI KATIKA KATA
ISHIRINI NA MOJA (21) ZA TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa ya uwepo wa nafasi wazi za udiwani kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, ameitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata 21 zilizopo katika Halmashauri 15 na Mikoa 10 ya Tanzania Bara.

Nafasi wazi za udiwani katika Kata hizo zimetokana na sababu mbalimbali zikiwepo Kifo, Kujiuzulu, kutohudhuria vikao na kufutwa uanachama.

Baada ya kupokea taarifa hiyo na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa; Tume ina utaarifu Umma kuhusu kuwepo kwa Uchaguzi mdogo katika Kata hizo 21.

Hivyo, Tume imepanga kuendesha Uchaguzi mdogo katika Kata hizo kwa kuzingatia Ratiba ifuatayo.

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 17 - 23 Agosti, mwaka huu,
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 23 Agosti, mwaka huu,
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kati ya tarehe 24 Agosti hadi tarehe 15 Septemba mwaka huu, na
4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 16 Septemba mwaka huu.

Kata zilizowazi na Halmashauri zake ni kama ifuatavyo:-

NA.	MKOA	HALMASHAURI		KATA
1.	ARUSHA	Halmashauri ya Wilaya ya Arusha	1	Kiutu
			2	Olturoto
		Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	3	Mswakini
2	DAR ES SALAAM	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	4	Zingiziwa
			5	Vingunguti
		Halmashauri ya Manispaa ya Temeke	6	Mbagala Kuu
3	DODOMA	Halmashauri ya Jiji la Dodoma	7	Kizota
4	GEITA	Halmashauri ya Wilaya ya Geita	8	Bugalama
5	KILIMANJARO	Halmashauri ya Wilaya ya Hai	9	Machame Uroki
			10	Kia
		Halmashauri ya Wilaya ya Siha	11	Nasai
6	KAGERA	Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi	12	Kashenye
7	MANYARA	Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto	13	Loorela
8	MBEYA	Halmashauri ya Jiji la Mbeya	14	Maanga
			15	Sisimba
			16	Iwambi
			17	Nsalaga
		Halmashauri ya Wilaya ya Kyela	18	Nkuyu
9	SIMIYU	Halmashauri ya Wilaya ya Meatu	19	Mwanhuzi
10	TANGA	Halmashauri ya Jiji la Tanga	20	Mwanzange
		Halmashauri ya Mji wa Korogwe	21	Masuguru

Kwa taarifa hii Tume inavialika Vyama vya Siasa, Wadau wote wa Uchaguzi na Wananchi kwa ujumla kushiriki katika Uchaguzi huo.

Mwisho, Tume inachukua fursa hii kuviisa Vyama vya Siasa na Wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia matakwa ya Katiba, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2015, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015 pamoja na maelekezo yote yaliyotolewa au yatakayotolewa na Tume wakati wote wa Uchaguzi mdogo.

Imetolewa leo tarehe 7 Agosti, 2018.



DKT. ATHUMAN J. KIHAMIA
MKURUGENZI WA UCHAGUZI